# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA

# TAARIFA YA UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA-TACCU

**S.L.P 1551, DODOMA.**

info@taccu.or.tz

## 1. UTANGULIZI

Umoja wa Makatibu wa kamati ulianzishwa kwa lengo la kuwaleta pamoja makatibu wote wa Kamati Tanzania bara. Kupata chombo cha pamoja cha kuwasemea, kutetea haki na maslahi yao ikiwa ni pamoja na kuthaminiwa mahala pa kazi, kubadilishana uzoefu na ujuzi katika kutekeleza vyema majuku yao ya kila siku. Taarifa hii itaonesha chimbuko la Umoja wa Makatibu wa Kamati, shughuli zilizofanyika na kufikiwa tangu kuanzishwa kwake na muelekeo wa Umoja wetu kwa ujumla.

## 2. CHIMBUKO NA USAJILI WA UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA

Chimbuko la Umoja wa Makatibu wa kamati lilianza rasmi mwaka 2023 ambapo wazo la uanzishwaji wake liliibuliwa na Makatibu walipokuwa kwenye Mafunzo ya kuwajengea uwezo Jijini Tanga, Makatibu wa Kamati waliazimia kuanzisha Umoja ambao utawaunganisha Makatibu wa Kamati wote Tanzania bara (Makatibu wa Kamati wa muundo na wale ambao wanatekeleza majukumu ya Katibu wa Kamati) ndipo hatua muhimu zilianza kuchukuliwa ili kukamilisha mchakato wa uanzishwaji wake.

Mwaka 2024, chini ya Uongozi wa mpito wa Kamati Tendaji Taifa, ukiongozwa na **Mawasiliano S. Deule** -Mwenyekiti wa Umoja huu kutoka Halmashauri ya Mji Mafinga, **Rukia Jaha** - Katibu wa Umoja kutoka Halmashauri ya Manispaa Mtwara, na **Fatuma Shams** - Muhasibu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino. Viongozi hawa kwa kushirikiana na Makatibu wa Kamati wengine waliojitolea Fedha na muda katika kufanikisha kusajili Umoja huu kwa jina la TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION (TACCU)- UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA. Chini ya sheria ya Msajili wa Vyama sura 337 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2002 na kupewa namba ya usajili **S.A.24065.**

## 3. KATIBA NA KANUNI ZA UMOJA.

Kama ulivyo utaratibu wa kisheria, usajili wa Umoja/Chama/Jumuiya yoyote lazima kuwe na Katiba na kanuni zake, hivyo viongozi waliandaa Katiba na kanuni ili kuendana na matakwa ya kisheria ya kusajili Umoja wa Makatibu wa Kamati. Kwa mara kadhaa katiba ya Umoja imewahi kurushwa katika kundi sogozi la TANZANIA COMMITTEE CLERK na kuibua mjadala mkubwa kuhusu mapungufu ya Katiba hiyo. Uongozi wa mpito utaandaa utaratibu mzuri wa kuratibu maoni na mapendekezo ili kufanya maboresho ya katiba ya sasa na hatimaye kupitishwa na wajumbe watakaohudhuria Mkutano mkuu wa kwanza unaotarajiwa kufanyika mwezi Agosti, 2026.

## 4. AKAUNTI YA BENKI YA UMOJA.

Uongozi ulifanikiwa kufungua akaunti ya Umoja kupitia beki ya NMB tawi la MAZENGO - Dodoma, na kupewa namba **51710092583** kwa jina la TANZANIA COMMITTEE CLERKS UNIONI. Tulikubaliana fedha zote zinakusanywa zifanyike kupitia akaunti hiyo. Watia saini wa akaunti hiyo ni Mawasiliano S. Deule ambaye ni Mwenyekiti, Rukia Jaha ambaye ni Katibu, Fatuma Shams

ambaye ni Muhasibu na Makandaiga Chacha ambaye ni Mjumbe wa Kamati Tendaji Taifa. Matumizi yote ya fedha za wanachama yanafuata sheria, kanuni, na taratibu za matumizi ya fedha za Umma, na taarifa ya mapato na matumizi itawasilishwa kwa wanachama wote kwa utaratibu wa vikao kama ilivyo ainishwa katika katiba na kanunu za umoja huu.

## 5. UONGOZI WA UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA.

Kwa sasa Umoja wa Makatibu wa Kamati Tanzania, unaongozwa na uongozi wa mpito chini ya Mwenyekiti Mawasiliano S. Deule, na viongozi wengine kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

**ORODHA YA VIONGOZI WA MPITO WA KAMATI TENDAJI TAIFA - TACCU**

| NA | JINA | CHEO | HALMASHAURI ATOKAYO | MKOA | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MAWASILIANO S. DEULE | MWENYEKITI | MAFINGA TC | IRINGA | 0762 622 090 |
| 2 | ISMAIL RASHIDI IDDI | MAKAMU M/KITI | NANYUMBU DC | MTWARA | 0652 638 400 |
| 3 | RUKIA JAHA | KATIBU | MTWARA MC | MTWARA | 0714 154 852 |
| 4 | EMMANUEL JUSTINE MGONJA | KATIBU MSAIDIZI | KISARAWE DC | PWANI | 0715 798 687 |
| 5 | FATUMA SHAMS | MUHASIBU | CHAMWINO DC | DODOMA | 0686 070 155 |
| 6 | MAKANDAIGA CHACHA MAGABE | MJUMBE | ITIGI DC | SINGIDA | 0762 030 036 |
| 7 | RAYMOND MBENA | MJUMBE | MANYONI DC | SINGIDA | 0784 154 395 |
| 8 | PETER YUSUPH MAIGE | MJUMBE | MISSENYI DC | KAGERA | 0767 644 442 |
| 9 | MELLO FAUSTINE RASSO | MJUMBE | DODOMA CC | DODOMA | 0767 326 849 |

**ORODHA YA WAJUMBE WAWAKILISHI WA MIKOA TANZANIA BARA - TACCU**

| NA | JINA | CHEO | HALMASHAURI ATOKAYO | MKOA | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SALUMU IBRAHIM UPETE | MJUMBE MWAKILISHI | IRINGA MC | IRINGA | 0683 380 331 |
| 2 | ISMAIL RASHIDI IDDI | MJUMBE MWAKILISHI | NANYUMBU DC | MTWARA | 0652 638 400 |
| 3 | ISMAIL HASAN JUMA | MJUMBE MWAKILISHI | UBUNGO MC | DAR ES SALAAM | 0767 686 734 |
| 4 | ANNASTAZIA SAMWEL BUJIKU | MJUMBE MWAKILISHI | KONGWA DC | DODOMA | 0765 563 322 |
| 5 | BONI BONI | MJUMBE MWAKILISHI | BUCHOSA DC | MWANZA | 0759 027 380 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 6 | EMMANUEL JUSTINE MGONJA | MJUMBE MWAKILISHI | KISARAWE DC | PWANI | 0715 798 687 |
| 7 | ALI OMARI MBAPAKIE | MJUMBE MWAKILISHI | NGARA DC | KAGERA | 0717 427 066 |
| 8 | WINFRIDA JULIUS ANTON | MJUMBE MWAKILISHI | SONGEA DC | RUVUMA | 0747 136 695 |
| 9 | GRACE GAMBADU | MJUMBE MWAKILISHI | MUSOMA MC | MARA | 0623 253 001 |
| 10 | SEBASTIAN MATHIAS MALEMBEKA | MJUMBE MWAKILISHI | NZEGA TC | TABORA | 0714 947 222 |
| 11 | WEMA YOHANA WILIUM | MJUMBE MWAKILISHI | KISHAPU DC | SHINYANGA | 0786 895 230 |
| 12 | MAKANDAIGA CHACHA MAGABE | MJUMBE MWAKILISHI | ITIGI DC | SINGIDA | 0762 030 036 |
| 13 | BABYANNA ALPHONCE NDUTAULA | MJUMBE MWAKILISHI | MONDULI DC | ARUSHA | 0774 191 309 |
| 14 | BONIFASIA BERNARD NDUNGURU | MJUMBE MWAKILISHI | NJOMBE DC | NJOMBE | 0754 727 670 |
| 15 | MANIFRED FAUSTINE JANGOLE | MJUMBE MWAKILISHI | CHATO DC | GEITA | 0769 127 055 |
| 16 | SAIDI HALIFA MVUNGI | MJUMBE MWAKILISHI | MOROGORO DC | MOROGORO | 0768 521 460 |
| 17 | JOSEPH DIDAS MLUNDI | MJUMBE MWAKILISHI | MBEYA CC | MBEYA | 0756 524 358 |
| 18 | AMANIEL MATOWO | MJUMBE MWAKILISHI | BUMBULI DC | TANGA | 0712 253 274 |
| 19 | HORTENSIA SAIBUNI REUBEN | MJUMBE MWAKILISHI | MASWA DC | SIMIYU | 0716 336 131 |
| 20 | AMINA MBWANA | MJUMBE MWAKILISHI | NACHINGWEA DC | LINDI | 0713 041 268 |
| 21 | CHRISPIN LYOBA | MJUMBE MWAKILISHI | TANGANYIKA DC | KATAVI | 0767 624 120 |
| 22 | HASSAN ISSA MAKANGE | MJUMBE MWAKILISHI | MOMBA DC | SONGWE | 0713 508 755 |
| 23 | RESTITUTER ANDREW MAKURU | MJUMBE MWAKILISHI | BABATI TC | MANYARA | 0767 503 947 |
| 24 | INNOCENT EKONY | MJUMBE MWAKILISHI | MOSHI MC | KILIMANJARO | 0717 406 089 |
| 25 | CHARLES AGAY MASHOMBELA | MJUMBE MWAKILISHI | KASULU TC | KIGOMA | 0762 344 707 |
| 26 | MARIA ISDORY NTARA | MJUMBE MWAKILISHI | SUMBAWANGA MC | RUKWA | 0765 814 560 |

## 6. UTAMBULISHO WA UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA.

Uongozi wa Umoja uliandika barua ya tarehe 22/01/2026 yenye Kumb. Namba TACCU/01/03 kwenda kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa lengo la kuutambulisha Umoja kwa ngazi ya Wizara, Mikoa na hadi Halmashauri zote nchini. Barua hiyo ilijibiwa kwa barua ya tarehe 31/03/2026 yenye Kumb. Na. JC.156/254.01C/1922 ambayo ilielekezwa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa ili ishuke kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote. Hadi sasa, barua za utambulisho zimeshafika kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kwa asilimia 80.

## 7. SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA

Mpaka kufika wakati huu, shughuli mbalimbali zimeendelea kutekelezwa na Viongozi. Kwa muhtasari shughuli hizo ni kama ifuatavyo.

i. Kuandika barua kwenda kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi kuhusu mapendekezo ya maboresho ya muundo wa kada ya Katibu wa Kamati katika mamlaka za Serikali za Mitaa, ikiwa ni pamoja na kuboreshwa kwa viwango vya mshahara katika kada hii. Barua hiyo ilijibiwa na kwa sasa mchakato wa maboresho upo katika hatua ya utekelezaji.

ii. Kuanza maandalizi ya awali ya kufanyika kwa Mkutano mkuu wa kwanza wa Umoja, ikiwa ni pamoja na kuandaa bajeti kuu ya Mkutano na kupitishwa na viongozi wote kupitia vikao vya kisheria vinavyofanyika kwa njia ya mtandao, kutafuta ukumbi ambapo Mkutano utafanyika, kuandika barua ya kuomba kibali cha kufanya Mkutano, kutafuta wadau/wadhamini wa Mkutano Mkuu, kuandika barua ya kumuomba Mgeni Rasmi na mlezi wa Umoja wetu.

iii. Kufungua email rasmi ya Umoja ambayo ni info@taccu.or.tz, kufungua ukurasa wa Instagram ambao unajulikana kwa jina la taccu_tanzania. Aidha taratibu za kufungua tovuti (Website) zinaendelea.

iv. Kuandaa kanzidata ya Makatibu wa Kamati. Ambapo katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara, Mikoa 19 imeshaandaa kanzidata na Mikoa 07 iliyosalia mchakato unaendelea

v. Kuhamasisha kuchangia ada ya unachama kupitia kwa viongozi wa Mikoa. Ada hizo ndiyo **zitamtambulisha mwanachama hai wa Umoja**, na inapaswa kulipwa kabla au ifikapo tarehe 30 Juni 2026. Ada hizi ndio zitasaidia katika michakato ya awali katika maandalizi ya kufanyika kwa Mkutano mkuu.

## 8. MWELEKEO WA UMOJA.

Umoja wa Makatibu wa Kamati Tanzania unatambua kuwa, Kada hii inaundwa na watu kutoka katika fani mbalimbali (Utawala, Utumishi, Sheria na kada zingine). Aidha Umoja huu unatambua kuwa wapo Makatibu wa Kamati ambao tayari wameshafanya mabadiliko ya muundo

(Recategorization). Wote hao wana sifa za kujiunga na Umoja huu, kwa kuwa lengo kuu ni kuwaunganisha wataalamu wote wanaotekeleza majukumu ya Katibu wa Kamati bila kujali cheo chake cha muundo.

Aidha Umoja unaendelea kufanya mawasiliano rasmi ya mara kwa mara na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kwa ajili ya kuboresha muundo wa kada hii, ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa kufanya kazi (Scope of work) ili kada isiishie katika Mamlaka za Serikali za Mitaa pekee, bali hata kweye Taasisi, Wizara, Bunge, Wakala wa Serikali, na Mashirika mbalimbali ya Serikali. Ili kufanikiwa katika hayo, ni lazima kuwepo na ushirikiano madhubuti kati ya Viongozi na wanachama na kufanya Mikutano ya kila mwaka.

## 9. MKUTANO MKUU WA KWANZA.

Kama ilivyoelezwa hapo awali, kwa sasa uongozi wa mpito wa Kamati Tendaji Taifa kwa kushirikiana na viongozi wa Mikoa na Maafisa kutoka Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Bunge, Sera, Uratibu na Wenye Ulemavu, unaendelea na maandalizi ya kufanyika kwa mkutano mkuu wa kwanza, ambapo Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkutano huo unatarajiwa kufanyika mwezi Agosti 2026 Jijini Dodoma, kwa muda wa siku tatu. Pamoja na mambo mengine, **Ajenda za Mkutano huo zitakuwa ni pamoja na; -**

i. Uzinduzi wa Umoja wa Makatibu wa kamati Tanzania
ii. Kufanya uchaguzi wa viongozi
iii. Kupitisha Katiba na kanuni za Umoja kama zitakavyofanyiwa maboresho na wajumbe.

Kulingana na kikao cha kupokea na kujadili rasimu ya bajeti kilichofanyika tarehe 11.04.2026 ilikubalika kuwa, mchango kwa kila mshiriki wa Mkutano huo utakuwa ni Tsh **550,000** na ada ya unachama ni Tsh **50,000**. Gharama za ushiriki zitagharamiwa na Wakurugenzi wa Halmashauri na ada ya uanachama itatolewa na mwanachama kabla au ifikapo Juni 30 2026. Aidha maandalizi yote ya Mkutano yanaendelea kuratibiwa na viongozi wote wa mpito kwa mgawanyo wa majukumu.

## 10. CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa hadi sasa bado Umoja wa Makatibu wa Kamati Tanzania unakabiliwa na changamoto mbalimbali, jitihada zinaendelea kuchukuliwa kwa lengo la kutatua na kuziondoa changamoto hizo. Aidha miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na hizi zifuatazo

i. Ukosefu wa Ofisi ya kudumu, Vitendea kazi vya Ofisi pamoja na mfanyakazi wa kuajiriwa atakayekuwa ofisini.
ii. Ukosefu wa fedha za kuendesha shughuli za Umoja, kutokana na kasi ndogo ya uchangiaji wa michango ya Ada na uwanachama.

iii. Kutowajibika kikamilifu kwa baadhi ya viongozi wa Mikoa.
iv. Mawazo hasi, yenye kukatisha tamaa na ya kuleta mgawanyiko kutoka kwa baadhi ya makatibu wa kamati pamoja na wajumbe wa kundi sogozi la Makatibu wa Kamati.

**11. UTATUZI WA CHANGAMOTO**

Uongozi umeendelea kuchukua hatua za kutatua changamoto zinazotukabili

i. Bajeti ya Mkutano Mkuu wa kwanza, suala la kupata kiwanja cha kujenga ofisi pamoja na kupata vitendeakazi vya Ofisi limezingatiwa
ii. Hamasa inaaendelea kutolewa kwa ngazi ya Mikoa ili kuhamasisha uchangiaji.
iii. Kufanya mabadiliko madogo ya viongozi wa Mikoa ambao hawatekelezi majukumu yao ipasavyo.
iv. Kuendelea kutoa uelewa kwa wajumbe kuhusu madhumuni na faida za kuwa na Umoja wa kada ya Katibu wa Kamati


**12. HITIMISHO.**

Mwisho uongozi unapenda kuwashukuru na kuwapongeza wale wote ambao walijitoa kwa fedha na muda wao na kufanikisha kufika hatua ulipo Umoja huu. Aidha Uongozi unawashukuru na kuwapongeza wale wote ambao wametoa michango ya Ada ya unachama. Kipekee kabisa uongozi unazishukuru Ofisi za Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora, na Ofisi ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia.

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Wabariki Makatibu wote wa Kamati Tanzania Bara, Mungu Ubariki Umoja wetu wa Makatibu wa Kamati Tanzania, Amina.

Naomba kuwasilisha,

Imetolewa na



**Mawasiliano S. Deule**

Mwenyekiti Umoja wa Makatibu wa Kamati Tanzania (TACCU)